



JUMUIYA YA KIKRISTO TANZANIA (CCT)

TAREHE: 07 FEBRUARI, 2025

TANGAZO LA ZABUNI YA ULINZI

Jumuiya ya Kikristo Tanzania ni Taasisi ya dini inayojulikana kwa kifupi kama CCT (Christian Council of Tanzania). ambayo ni muunganiko wa makanisa, Wanachama, na mashirika ya Kikristo Tanzania. Makao Makuu ya Jumuiya ya Kikristo yapo Dodoma.

CCT inapenda kuwatangazia Wazabuni wote wenye Makampuni, ambayo yanatoa huduma za Ulinzi kuwa tunatangaza nafasi hii ya kutoa huduma za **ULINZI** wa ofisi katika Taasisi yetu iliyopo Dodoma Makao Makuu.

A. SIFA ZA KAMPUNI: -

- 1) Iwe ni Kampuni inayofahamika na yenye uaminifu katika kazi yake
- 2) Wafanyakazi wake wawe wamepitia Jeshi, ama mafunzo ya mgambo au ulinzi na kutunukiwa cheti
- 3) Walinzi wawe na uzoefu katika ulinzi na doria
- 4) Kampuni iwe na wadhamini wasiopungua wawili
- 5) Walinzi wa kampuni wawe na uzoefu wa kukabilia na mhalifu yeyote katika eneo lake la kazi
- 6) Walinzi wawe na uzoefu wa kutumia silaha ama kitendea kazi (silaha) pindi anapokutana na tatizo

B. MWOMBAJI (KAMPUNI) AELEZE KWENYE BARUA YAKE NA KUAMBATANISHA VIFUATAVYO: -

- 1) Kampuni iwe na Cheti cha Usajili kinachotambulika na Mamlaka nchini Tanzania.
- 2) Nakala ya mahali ambapo mmeshafanya nao kazi (Profile)
- 3) Nakala ya kitambulisho cha Taifa au cha mpiga kura kwa mmiliki/wamiliki
- 4) Mawasiliano ya wadhamini wasiopungua wawili wanaofahamika na wenye makazi ya kudumu;
- 5) Leseni ya Biashara

Mawasiliano:

Kila muombaji aweke anuani sahihi ambayo anaitumia kwa mawasiliano yake. Pia aweke Namba ya simu sahihi anayoitumia muda wote na barua pepe.

Jinsi ya kutuma maombi:

Maombi ya kazi tajwa hapo juu yatumwe kwa anuani iliyoonyeshwa hapa chini.

Katibu Mkuu,
Jumuiya ya Kikristo Tanzania - CCT,
S. L. P. 1454,
DODOMA.

Au maombi yapelekwe kwa mkono ofisi za mapokezi za **CCT - Dodoma** ambazo zipo barabara ya Hospitali, Mkabala na Jengo la Mackay na Mkapu House (**ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma**).

Mwisho wa kutuma maombi:

Mwisho wa kutuma maombi ni Jumatatu tarehe 18 Februari, 2025 saa 9:00 Alasiri.

KATIBU MKUU
CCT – MAKAO MAKUU DODOMA